SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

# TAARIFA YA TAHADHARI KWA WANACHAMA

## KUSUDIO LA SCANCEM INTERNATIONAL DA YA KUNUNUA ASILIMIA 68.33 ZA TANGA KUTOKA AFRISAM MAURITIUS INVESTMENT HOLDINGS LIMITED

## TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY (DSE: TCPLC)

**(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ("Tanga" au "Kampuni")**

Wanahisa wanakumbushwa kuhusu tangazo lililotolewa na HeidelbergCement AG ("Heidleberg Cement) na AfriSam Mauritius Investment Holdings Limited ("AfriSam") tarehe 26 Oktoba 2021 (tangazo la HeidelbergCement) ambapo ilitangazwa kuwa Scancem International DA ("Scancem"), kampuni tanzu ya HeidelbergCement, na AfriSam wamekamilisha makubaliano ambapo Scancem itanunua asilimia 68.33 ambazo ni hisa za AfriSam ndani ya Tanga Cement PLC, ("Mnunuzi"). Wanahisa wanahimizwa kusoma matangazo ya pamoja yanayotolewa na AfriSam na HeidelbergCement.

Bodi ya wakurugenzi ya Tanga ("Bodi) ilifahamishwa vyema na AfriSam kuhusu mapatano ya uuzwaji muda mfupi baada ya makubaliano kukamilika. Kwasasa Bodi itachukua na kufuata ushauri muafaka na kufuata hatua zinazohitajika kwenye masuala ya Soko la Mitaji na Dhamana na kufuata kanuni za (Ununuzi wa kuchukua, Uchukuaji na Muunganisho) za mwaka 2006. Bodi itatoa maelezo zaidi kwa wanahisa wake kwa wakati muafaka kuhusu suala hili.

Ununuzi utategemea kutimizwa, au ikiwezekana, kuondolewa kwa masharti ("Masharti") ifikapo tarehe 30 Juni 2022 au tarehe ya baadaye endapo wahusika watakubaliana kimaandishi. Masharti haya yamewekwa kwa kina katika tangazo la pamoja baina ya AfriSam na HeidelbergCement. Bei elekezi kwa kila hisa itakayolipwa na Scancem kwenda AfriSam ni Tzs 3,157 kwa hisa ya Tanga ("Bei ya Ununuzi"). Bei ya Ununuzi pia inategemea marekebisho yanayoendana na deni, mtaji wa kufanyia kazi na gharama nyingine. HeidelbergCement na AfriSam inatahadharisha kuwa hakuna uhakika wa makubaliano ya Bei ya mwisho ya Ununuzi.

Endapo ununuzi huu utakuwa bila ya masharti na kutekelezwa, Scancem itachukua udhibiti wa kampuni. Endapo hili litatokea, Scancem itatoa ofa ya jumla ya ununuzi wa hisa zilizobakia za Tanga ("Ofa ya Jumla"); hilo litafanyika baada ya kufikiwa kwa makubaliano ya mwisho ya ununuzi, na bei itafahamika.

Wanahisa wanatahadharishwa kuwa hakuna uhakika kwamba masharti yote ya ununuzi yatatekelezwa au kushindikana. Hivyo, hakuna uhakika kuwa ofa ya jumla itatolewa. Vilevile hakuna uhakika wa makubaliano ya bei ya mwisho ya ununuzi.

Kampuni bado inaendelea kufanya biashara huku kukiwa na tangazo la tahadhari lililotolewa mnamo tarehe 31 Agosti 2021. Wanahisa wanashauriwa kuendelea kuwa wangaalifu wanapojishughulisha na biashara ya dhamana za Tanga.

Taarifa zaidi zitaendelea kutolewa kwa muda muafaka.

**Kwa niaba ya Bodi**

**Mwenyekiti wa Bodi**
Chairman of the Board
27 Oktoba 2021

**KUSUDIO LA SCANCEM INTERNATIONAL DA KUNUNUA ASILIMIA 68.33 YA HISA ZA TANGA CEMENT PLC (“TANGA CEMENT”), KAMPUNI ILIYOSAJILIWA NA WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA) KWA NAMBA 5068 NA INAYOENDESHWA KWA MUJIBU WA SHERIA ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Kampuni ya Scancem International DA (“Scancem”), kampuni tanzu ya HeidelbergCement AG (“HeidelbergCement”) na Afrisam Mauritius Investment Holdings Limited (“Afrisam”) zimeafikiana kwamba Scancem itanunua asilimia 68.33 ya hisa za Tanga Cement (“Ununuzi”). Ununuzi huu utategemea utekelezaji wa au kusamehe kutekeleza, vyovyote inavyofaa, masharti ya msingi (“masharti”) ifikapo tarehe 30 Juni 2022 au tarehe nyingineyo itakayokubaliwa na pande zote.

Bila ya kuathiri makubaliano ya mwisho kati ya Scancem and Afrisam (“bei ya ununuzi”), bei ya hisa moja itakayolipwa na Scancem kwa Afrisam ni TZS 3,157 na hivyo kufanya jumla ya fedha itakayolipwa kuwa TZS 137,329 milioni kwa hisa zote, yaani asilimia 68.33, zinazomilikiwa na Afrisam kwenye kampuni ya Tanga Cement. Bei ya ununuzi yaweza kuathiriwa na marekebisho yanayohusu madeni, mtaji wa kufanyia kazi, matumizi mengine na uwezekano wa marekebisho mengine baada ya kufungwa kwa ununuzi. Hivyo basi, ni muhimu kutambua kwamba, kwa sasa hakuna uhakika juu ya bei ya mwisho ya ununuzi wa hisa.

Masharti ya msingi yanayotakiwa kutekelezwa kabla ya kukamilisha ununuzi ni pamoja na; (i) Ruhusa ya Tume ya Ushindani Tanzania (“FCC”) kwamba ununuzi umekubaliwa kwa vigezo vinavyokubalika na pande zote, (ii) Ruhusa ya Tume ya Madini Tanzania, (“TMC”) kwamba ununuzi umekubaliwa kwa vigezo vinavyokubalika na pande zote, (iii) Ruhusa ya wanahisa wa Tanga Cement juu ya ununuzi kukubaliwa kwa azimio maalum la wanahisa (special resolution) kwenye mkutano maalumu wa wanahisa ulioitishwa kama inavyotakiwa chini ya Kanuni 9(5) ya Kanuni za Ununuzi Mkubwa, Utwaaji na Muunganiko kwenye Masoko ya Mitaji na Dhamana za mwaka 2006 (“Kanuni”), (iv) Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa cheti cha uthibitisho kuwa kodi inayohusiana na ununuzi/uuzaji huu wa hisa imelipwa, (v) Baadhi ya leseni za madini zilizotolewa kihalali au zimeombwa upya na Tanga Cement, (vi) Ruhusa ya Idara ya ufuatiliaji wa fedha ya Benki ya Hifadhi ya Afrika ya Kusini au kama inaruhusiwa, Muuzaji alieruhusiwa, kuhusika na wajibu wa Afrisam (South Africa) Proprietary Limited, ambayo ni kampuni tanzu ya AfriSam Holdings (Pty) Ltd (“AfriSam Group”) kama mdhamini kuhusu ununuzi, kutolewa.

Endapo masharti yote yatatekelezwa au yatasamehewa kutekelezwa mapema, basi ununuzi hautakuwa na masharti na hivyo utatekelezwa, ambapo utekelezwaji unatazamiwa kufanyika mapema katika robo ya pili ya mwaka 2022.

Endapo ununuzi utakuwa hauna masharti na ukatekelezwa, utaifanya kampuni ya ScanCem kuwa mmiliki mkubwa wa Tanga Cement. Endapo hili litatokea na kama inavyotakiwa na Kanuni kuu ya pili ya Kanuni tajwa hapo juu, Scancem, baada ya bei ya mwisho ya ununuzi kuwa imeamuliwa, itapeleka ofa ya jumla kwa Tanga Cement ya kutwaa hisa zilizobaki (Ofa ya jumla). Ofa ya jumla inatakiwa kuruhusiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Tanzania (“CMSA”). Ili kuhakikisha kwamba wanahisa wote wa Tanga Cement wanapokea kiasi sawa na bei ya hisa iliyolipwa na Scancem kwa Afrisam kulingana na ununuzi kama inavyotakiwa na Kanuni/sheria, ofa ya jumla itapelekwa tu baada ya kuamua bei ya mwisho itakayolipwa na Scancem kwa Afrisam.

Pande zote mbili zinaendelea kufanya mazungumzo na mamlaka za usimamizi, ikiwemo CMSA, Soko la Hisa la Dar es Salaam (“DSE”), FCC na TMC kuhusu ununuzi huu. Matamko mengine yatafuata kadri mazungumzo yatakavyokuwa yanaendelea.

Wanahisa wa Tanga Cement wanatahadharishwa kwamba hakuna hakikisho kuwa masharti yote yatatekelezwa au kusamehewa kutekelezwa kwa wakati. Hivyo basi, hakuna uhakika kama ofa ya jumla itapelekwa. Wanahisa

wanashauriwa kuchukua tahadhari wanapofanya lolote kuhusiana na hisa zao kwenye kampuni ya Tanga Cement mpaka pale tangazo litakapotolewa kuhusu kukamilika kwa ununuzi.

*Kuhusu HeidelbergCement*

HeidelbergCement ni moja ya makampuni makubwa duniani yanayojihusisha na utengenezaji wa vifaa vya ujenzi. Kampuni ni kinara katika soko la uuzaji wa kokoto, saruji na zege iliyochanganywa tayari. Ina wafanyakazi takribani 53,000, katika sehemu zaidi ya 3,000 na kwenye nchi zaidi ya 50. Kampuni ina rekodi ya muda mrefu ya kufanya vizuri kifedha kutokana na utendaji bora wenye uwazi katika kupokea mabadiliko. HeidelbergCement inatambua umuhimu wa uwajibikaji katika kutunza mazingira. Ikiwa kinara wa kupunguza athari za hewa ya ukaa (kaboni), HeidelbergCement inatengeneza vifaa suluhishi katika kudhibiti athari za hewa hiyo katika nyakati zijazo. Nchini Tanzania, HeidelbergCement imekuwepo kwa muda mrefu kupitia kampuni yake tanzu ya Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC), iliyoanzishwa mwaka 1966.

*Kuhusu AfriSam*

AfriSam ni msambazaji mbobezi wa vifaa bora vya ujenzi na mbinu za kiufundi. Vifaa vya ujenzi kama saruji na zege iliyochanganywa tayari (RMC) ya AfriSam imechangia sana kwenye maendeleo ya miundombinu barani Afrika kwa zaidi ya miaka 85. Afrisam iko nchini Tanzania kupitia Kampuni ya Tanga Cement ambayo ni mzalishaji wa saruji ya chapa Simba.

AfriSam
Creating Concrete Possibilities

HEIDELBERGCEMENT